

Kujifunza kutoka nyumbani ikiwa shule inafungwa

Habari kwa wazazi na walezi

Ikiwa shule ya mtoto wako inahitaji kufunga, shule watawasiliana na familia kwa kutumia njia zake za kawaida (hii inaweza kuwa kupitia barua pepe, SMS, tovuti).

Ikiwa shule zimefungwa kwa muda mrefu, shule itaendelea kutoa shughuli za kujifunza kwa mtoto wako kufanya nyumbani na watawasiliana na wewe juu ya kujifunza kwao.

Katika shule nyingi kote katika jimbo walimu tayari hutolea na kusimamia shughuli za masomo kwa kutumia zana za mtandao. Shule zingine zinaweza kusonga mtandaoni shughuli zaidi au zote za kujifunza kwa mtoto wako. Hii inaweza ikiwemo masomo mengine ya moja kwa moja. Ikiwa wewe au shule yako haina chaguzi za dijiti au mtandaoni watatumia mikakati isiyo ya dijiti. Hii inaweza kuwemo kutuma jarida, vitabu vya maandishi au vinjari za USB zenyenye karatasi za shughuli za dijiti pamoja na video kwa nyumbani kwako kubebwa na mtoto wako au kwa barua.

Walimu wanaweza pia kuwasiliana na wanafunzi katika vikundi au kupitia simu mmoja kwa mmoja.

Karatasi ya habari itakusaidia kuelewa jinsi ya kumsaidia mtoto wako kujifunza nyumbani pamoja na:

- Majukumu yako - kuna mambo utahitaji kuyafanya ili kumsaidia mtoto wako kujifunza nyumbani kama vile kuweka utaratibu, kupata mahali pa kimya na kuuliza jinsi masomo yao yanavyoendelea.
- Majukumu ya mtoto wako - mtoto wako pia atahitaji kufuata utaratibu uliowekwa kwa ajili yake na kumaliza shughuli ambazo mwalimu anampa wakati anaposoma vizuri.
- Jinsi ya kupanga siku yake - shule yako inapaswa kukupa ushauri kadhaa na mwongozo kwa shughuli ambazo mtoto wako anapashwa kuzifanya mnamo siku.
- Kutunza ustawi wao – utahitaji kuhakikisha wana mapumziko, wanakunywa maji na hawaangukiwi au kuwa na wasi wasi.
- Mawasiliano - itakuwa muhimu uongee na mtoto wako kila mara juu ya masomo yake. Mwalimu wa mtoto wako na/au shule watawasiliana nawe na watakuambia jinsi ya kuwasiliana nao.
- Kutumia wakati wa teknolojia na skrini - itakuwa muhimu kumsimamia mtoto wako kutumia teknolojia kwa usalama na uweke mipaka kwa wakati wanaotumia mtandaoni.

Huduma ya Ukalimani wa Simu

Ikiwa unahitaji habari zaidi tafadhali piga simu kwa mwalimu mkuu wa shule yako. Ikiwa unahitaji mkalimani kukusaidia na swali lako tafadhali piga simu Huduma ya Ukalimani wa Simu kwenye 131 450 na uombe mkalimani wa lugha yako. Huduma hii itakuwa ya bure kwako.